**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**
**WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE**

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE

**MHESHIMIWA SIMAI MOHAMMED SAID (MBM),**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA, KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

**MEI, 2023.**

## YAKIYOMO


YALIYOMO ........................................................................i

VIFUPISHO VYA MANENO ................................................iv

A. UTANGULIZI.................................................................1
B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA......................3
MUUNDO WA WIZARA..................................................3
MAJUKUMU YA WIZARA...............................................3
C. MAFANIKIO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA .
2022/2023 ...........................................................................4
SEKTA YA UTALII ...........................................................4
SEKTA YA MAMBO YA KALE .........................................8
CHANGAMOTO ZA WIZARA.......................................10
a.Mapato yaliyokusanywa na Wizara kwa kipindi cha
miezi tisa (Julai 2022-Machi 2023) ..............................11
b. Fedha iliyopatikana kwa kipindi miezi tisa
(Julai 2022-Machi 2023)..............................................11
D. PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA
MAMBO YA KALE ......................................................12
Programu Kuu za Wizara................................................12
Programu ndogo za Wizara ............................................12
E. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO
KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ...........................13
F UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI
ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI
2022-MACHI 2023...........................................................13
1. PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO,
MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE
.................................................................................14
UTEKELEZAJI HALISI ..............................................14

2. PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII........19
UTEKELEZAJI HALISI........20
3. PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII........22
UTEKELEZAJI HALISI........22
4. PROGRAMU YA KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII........24
UTEKELEZAJI HALISI........24
UTEKELEZAJI HALISI........25
5. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE........27
UTEKELEZAJI HALISI........28
UTEKELEZAJI HALISI........29
UTEKELEZAJI HALISI........31
G. VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024........33
H. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024........33
I. KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU (PROGRAM BASED BUDGET - PBB) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024........34
Programu ya Kwanza: Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe........35
Programu ya Pili: Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii........36
Programu ya Tatu: Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii........37
Programu ya Nne: Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii........38

Programu ya Tano: Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale ........................................... 40

J. SHUKURANI ......................................................... 43

K. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ......................................................... 46

L. HITIMISHO ......................................................... 47

VIAMBATISHO ......................................................... 48

# VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| 1. | CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| 2. | DKT | Daktari |
| 3. | DW | Deutsche Well |
| 4. | EBS | Education Broadcasting System |
| 5. | FM | Frequency Modulation |
| 6. | ITB | Internationale Tourismus Borse |
| 7. | MBM | Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi |
| 8. | MoU | Memorundum Of Understanding |
| 9. | SMIDA | Small and Medium Industrial Development Agency |
| 19. | SMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| 20. | SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| 10. | TBC | Tanzania Broadcasting Cooperation |
| 11. | TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| 12. | Tv | Television |
| 13. | USA | United States of America |
| 14. | UNESCO | United Nations, Educational, Scientific, and Cultural Organization |
| 15. | UNICEF | United Nations International Children Emergency Funds |
| 16. | UNDP | United Nations Development Programme |
| 17. | UNECA | United Nations Economic Commissions for Africa |
| 18. | UNWTO | United Nations World Tourism Organization |
| 19. | UVIKO | Ugonjwa Unaosababishwa na Virusi vya Korona |
| 20. | ZABESA | Zanzibar Body Exercise Sports Association |
| 21. | ZBC | Zanzibar Broadcasting Cooperation |
| 22. | ZTITE | Zanzibar Tourism Investment And Travel Exhibition |
| 23. | ZATI | Zanzibar Association for Tourism Investors |
| 24. | ZATO | Zanzibar Association for Tourist |

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE, MHESHIMIWA SIMAI MOHAMMED SAID (MBM), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA, KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu muumba wa Mbingu na Ardhi kwa kuendelea kuturuzuku uzima na uhai pamoja na kutuwezesha kukutana tena leo, ili tuweze kujadili utekelezaji wa Malengo na Majukumu ya Wizara kwa kipindi cha miezi tisa. Kazi hii inatekelezwa kwa manufaa mapana ya wananchi wa Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze vyema katika kutekeleza jukumu hili, huku tukitanguliza mbele maslahi ya Taifa letu.

2. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuijenga Zanzibar na kuwapatia wananchi wake maendeleo makubwa kwa kipindi kifupi alichokuwepo madarakani. Hii imedhihirika wakati wa uwekaji wa Mawe ya Msingi pamoja na Uzinduzi wa Miradi ya Maendeleo tofauti katika kipindi cha shamra shamra za kuadhimisha miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa pande zote za Unguja na Pemba. Aidha, niendelee kumpongeza kwa kuitekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 - 2025, ambayo inalenga kuleta mageuzi makubwa katika nchi yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu afya njema pamoja na

kumzidishia Hekima, Maarifa na Uadilifu wakati akiendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako, nampongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais, kwa kuchapa kazi kwa kiwango cha hali ya juu na kumsaidia Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya nchi pamoja na kuendelea kuibakisha nchi yetu katika hali ya Umoja, Upendo na Mshikamano huku tukijivunia Amani na Utulivu uliotawala.

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii adhimu, kukupongeza wewe Spika wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Wasaidizi wako wote akiwemo Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza, Katibu wa Baraza, Wajumbe wa Baraza, Maofisa na Wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa jitihada za hali ya juu wanazozitumia katika kufanikisha majukumu ya Baraza hili. Aidha, nichukuwe fursa hii ya kutoa mkono wa pole kwa familia ya aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe, Mheshimiwa Habib Ali Mohammed aliyefariki tarehe 03/03/2023. Ninamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema Peponi, Amin.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kilimo, Biashara na Utalii ikiongozwa na Mwenyeketi mahiri Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi na Makamu Mwenyeketi Mheshimiwa Aza Januari Joseph pamoja na wajumbe wake wote kwa maelekezo, ushauri na Miongozo makini wanayotupa wakati wa kutekeleza Majukumu na Miradi ya Maendeleo ya Wizara. Mimi binafsi na watendaji wenzangu wote tunafarijika sana kwa kuwa nao na kwa kushirikiana vizuri katika utekelezaji wa kazi zetu.

## B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

6. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imeundwa kwa lengo la kusimamia Sekta Kuu mbili ambazo ni Utalii na Mambo ya Kale. Vile vile, Wizara hii imepewa majukumu ambayo huyatumia katika kupanga malengo ya Idara na Taasisi zetu.

### MUUNDO WA WIZARA

7. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inasimamia Taasisi na Idara zifuatazo: -

   i. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
   ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
   iii. Idara ya Utalii
   iv. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale
   v. Ofisi Kuu Pemba
   vi. Kamisheni ya Utalii Zanzibar
   vii. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe

### MAJUKUMU YA WIZARA

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na mambo mengine pia inatekeleza majukumu yafuatayo: -

   i. Kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

   ii. Kukuza pato la nchi kupitia Sekta ya Utalii.

   iii. Kuwashawishi wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuanzisha miradi ya utalii itakayotoa tija kwa wananchi.

   iv. Kuyalinda, kuyahifadhi na kuyatangaza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini.

v. Kuvitunza vitu na mabaki ya kihistoria yaliyopo nchini ili kuweka kumbukumbu kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

vi. Kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar.

## C. MAFANIKIO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na mambo mengine imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

## SEKTA YA UTALII

i. Wizara imeshiriki kwenye ziara za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi za Oman na Saudia (Kushiriki kwenye Mkutano 'World Tourism Council') kwa lengo la kuboresha uhusiano wetu lakini pia kuhudhuria mikutano mbali mbali ya kimataifa kutangaza fursa zilizopo za utalii na uwekezaji kwa ujumla. Aidha, uongozi wa Wizara ulipata fursa kushiriki Mkutano wa UNESCO wa kila mwaka kuongelea masuala ya Uhifadhi na Uendelezaji wa maeneo ya Urithi na Mambo ya Kale, hususan Mji Mkongwe.

ii. Baada ya kutagazwa kwa maradhi ya Marburg Tanzania, Wizara ilichukua juhudi za makusudi kwa kushirikiana na Taasisi binafsi na vyombo vya Habari vya Kitaifa na Kimataifa, kuwahakikishia wageni kuwa Zanzibar ipo salama, ambapo matoleo tofauti na vipindi zaidi ya 10 viliwahakikishia wageni juu ya usalama wao wakiwa Zanzibar. Zoezi hili kupitia vyombo vya habari limepelekea kutoathirika kwa shughuli za Kitalii Zanzibar, ikilinganishwa na kipindi cha UVIKO 19 .

iii. Wizara kwa kushirikiana na wadau wa utalii imefanikiwa kuandaa Maonesho ya kwanza ya Utalii na Uwekezaji "Zanzibar Tourism Investment and Travel Exhibition" (ZTITE) yaliyofunguliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika jengo la Beit al Aman Mnazimoja. Katika maonesho hayo yaliyowakutanisha wanunuzi na wauzaji wa huduma za utalii wa kitaifa na kimataifa kwa lengo la kukuza utalii endelevu wa Zanzibar. Maonesho hayo yalizindua Kampeni ya Kuifanya Zanzibar ya Kijani 'Greener Zanzibar'. Aidha, Makongamano na Mikutano mbali mbali yamefanyika. Kufanyika kwa maonesho haya kunafunguwa milango kwa Zanzibar katika suala la uwekezaji kwenye sekta ya utalii na kutangazwa zaidi katika masoko ya utalii ndani na nje ya nchi.

iv. Wizara kupitia Kamisheni ya Utalii imeshinda Tunzo ya Bodi Bora ya Utalii Afrika 2022 (Best African Tourism Board 2022) iliyotolewa huko Lagos - Nigeria na Pyne Awards 2022 na kupokelewa na Mwenyeketi wa Bodi ya Kamisheni ya Utalii Nd. Rahim Mohamed Bhaloo. Kushinda kwa tunzo hii kunadhirisha umahiri na ubora wa utendaji kazi wa bodi zetu Kitaifa na Kimataifa.

v. Wizara kupitia Kamisheni ya Utalii imeshinda Tunzo ya 'World Travel Awards' 2022, kwa kuwa Kituo Bora cha Utalii wa Fukwe kwa Afrika, 'Africa's Leading Beach Destination'. Tunzo za 'World Travel Awards' hutolewa kila mwaka ili kutambua na kutunuku ubora katika sekta ya Usafiri na Utalii ulimwenguni na kuaminiwa kuwa tunzo zenye hadhi kubwa katika tasnia ya usafiri na Utalii.

vi. Wizara imefanikiwa kushiriki katika Maonesho ya Utalii ya Kimataifa kama vile ITB (Internationale Tourismus Börse) – Berlin na Maonesho ya Wazi (Road Show) katika nchi za Ujerumani (Cologne), Uholanzi (Amsterdam), Ubelgiji (Brussels) na Ufaransa (Paris). Aidha, Wizara imeshiriki katika maonesho ya utalii ya Kitaifa kama vile Swahili Expo (SITE) - Dar –es- salaam na Kili Karibu Fair – Arusha.

vii. Kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini mwaka 2022 kwa asilimia 39 kutoka watalii 394,185 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 548,503 mwaka 2022. Hii inatokana na juhudi zinazochukuliwa na Wizara katika kuitangaza nchi Kitaifa na Kimataifa. Aidha, siku za ukaazi kwa wageni zimeongezeka kutoka siku saba (7) kwa mwaka 2019 hadi kufikia siku nane (8) kwa Machi, 2023.

viii. Wizara imefanikiwa kuialika Kampuni ya EBS kutoka Korea ya Kusini ambayo imeandaa makala (documentary) za vivutio vya utalii vya Zanzibar ambazo zimeoneshwa katika mitandao ya kijamii na televisheni. Aidha, Wizara imewapokea watu mashuhuri wakiwemo Muigizaji maarufu kutoka Hollywood- Marekani Lupita Nyong’o na msanii mashuhuri Bw. Maher Zain. Kuja kwa watu hawa maarufu nchini kunachangia kuitangaza Zanzibar Kimataifa pamoja na kuongeza idadi ya wageni nchini.

ix. Wizara imepokea meli tano kubwa za kitalii ambazo ni Zaandam, MS Coral, Geographer, Le Jacques Cartier na MV Seaborne. Meli hizo ziliwasili nchini na kushusha watalii elfu mbili (2000) ambao wamepata fursa ya kuvitembelea vivutio mbali mbali vya kitalii ikiwemo mashamba ya viungo, Msitu wa Jozani na maeneo ya Mji Mkongwe.

x. Wizara kupitia Kamisheni ya Utalii kwa upande wa Pemba imefanikiwa kuongeza idadi ya watalii walioingia Kisiwani humo kutoka watalii 14,548 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 27,826 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 91.

xi. Wizara inaendelea kukiimarisha Kikosi cha Polisi Utalii na Diplomasia kwa kukitengenezea Nguvu za Kisheria pamoja na kuwapa mafunzo askari hao ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kikosi kimefanya doria maalum kumi na mmoja (11). Kuwepo kwa kikosi hichi kumezidi kuongeza hali ya utulivu kwa wageni na kupunguza uhalifu katika maeneo ya kisiwa cha Unguja Kaskazini na Kusini. Aidha, Wizara itakizindua kikosi hichi rasmi kwa upande wa Pemba mwaka wa fedha 2023/2024.

xii. Wizara imeendelea kufanya Tamasha la Michezo la Utalii Pemba 'Tourist Sports Bonanza' ili kushajihisha maendeleo ya utalii kisiwani humo, ambalo limeshirikisha resi za ngarawa, mbio za baskeli, mashindano ya dufu na mashindano ya riadha.

xiii. Kuongezeka kwa idadi ya watazamaji wa filamu ya 'Royal Tour' ambayo imevunja rekodi kuliko 'Royal Tour' zote za nchi nyengine zilizowahi kufanyika, ambapo zaidi ya watu bilioni 1.2 duniani wameitazama filamu hiyo. Kamati ya Uandaaji wa Filamu imefanikiwa kutafsiri filamu hiyo kwa lugha ya Kichina na inaenedelea na kazi ya kuifanyia tafsri kwa lugha nyengine ili itazamwe na watu wengi zaidi.

xiv. Jarida la Safari duniani lijulikanalo kama 'The Travel' limetangaza Zanzibar kuwa kituo bora zaidi cha likizo ya majira ya joto 'Top Summer Destination in Africa' ikishindana na maeneo maarufu kama vile Cape Town (Afrika Kusini) na Piramidi za Giza (Misri).

## SEKTA YA MAMBO YA KALE

i. Mkataba wa ujenzi wa jengo la Beit el Ajaib liliopo Forodhani Unguja umesainiwa tarehe 13/02/2023 baina ya Serikali ya Ufalme wa Oman na kampuni ya Nandhra Engineering and Construction Company Limited ya Tanzania na utagharimu Dola Milioni 21 za Kimarekani. Mkandarasi wa ujenzi huo ameshakabidhiwa jengo na hivi sasa yupo katika matayarisho ya kuanza ujenzi huo. Ujenzi unaotarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu, utarudisha haiba na mvuto wa awali wa eneo hili na kupelekea wenyeji na wageni wengi kulitembelea eneo hili kwa ajili kupata historia kamili.

ii. Wizara kupitia Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imeshiriki katika utafiti mkubwa wa akiolojia ndani ya jengo la Ngome Kongwe, ulioongozwa na Profesa Mark Horton wa Chuo Kikuu cha Royal Agriculture University ya Cirencester nchini Uingereza. Utafiti huo umesaidia kwa kiasi kikubwa kuifahamu asili ya Zanzibar na historia ya eneo hilo. Aidha, mabaki mbali mbali yamegunduliwa yakiwemo mabaki ya nyumba za udongo za Waswahili wa karne ya 11 kabla ya kufika Wareno na Waarabu Zanzibar. Vile vile, mabaki ya watu wenye asili ya Ureno pamoja na msingi wa Kanisa la Karne ya 16 yamegunduliwa. Utafiti huo umesaidia kufahamu kuwa eneo la Ngome Kongwe lina historia ya takribani miaka 800 zaidi kuliko inavyofahamika sasa. Huu ni ugunduzi mkubwa kwa mara ya kwanza kwenye historia ya Zanzibar.

iii. Wizara imeratibu mkutano mkubwa wa Wanaakiolojia kutoka nchi za Afrika 'Pan African Archeological Conference', uliofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Utalii Maruhubi. Mkutano huo umewashirikisha watafiti wa Mambo ya

Kale takriban 300 kutoka nchi tofauti duniani. Watafiti hao waliwasilisha matokeo ya tafiti mbali mbali walizozifanya katika nchi za Afrika Mashariki ikiwemo Zanzibar. Matokeo hayo yameisaidia Wizara kuelezea uhalisia wa historia ya Zanzibar.

iv. Wizara kwa kupitia Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imeingia Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Prussian Cultural Heritage Foundation na Chuo cha Utafiti Dahlem zilizopo nchini Ujerumani kuendeleza mashirikiano ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa pande zote mbili.

v. Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kupitia Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ilitangaza fursa ya uwekezaji katika eneo la Mji Mkongwe kwa kuzingatia kwamba tayari yapo majengo 127 yaliyo katika hali mbaya ili kuyaimarisha. Hadi hivi sasa, majengo 14 yameshakabidhiwa wawekezaji, ambapo majengo sita tayari yameshaanza kufanyiwa matengenezo.

vi. Wizara imefanya tathmini ya gharama za matengenezo ya majengo 36 yaliyo katika hali mbaya zaidi ambapo jumla ya Shilingi bilioni 22,201,837,350/= zinahitajika ili kuyarejesha majengo hayo katika hali iliyo bora. Aidha, Wizara imeshatayarisha michoro ya nyumba 10 kati ya 36 zilizo katika hali mbaya zaidi kwa lengo la kuzinusuru zisije kuanguka. Aidha, makisio na michoro hiyo imewasilishwa Serikalini ili kuchukuliwa hatua zinazofaa. Mchakato wa muendelezo wa kuandaa michoro ya nyumba zilizobakia unaendelea.

vii. Wizara kupitia Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imeweza kuongeza vyanzo vipya viwili vya mapato, ambavyo

ni Kisiwa cha Changuu na Kanisa la Anglikana. Kuwepo kwa vyanzo hivi kutasaidia kuongezeka ukusanyaji wa mapato ya Wizara.

viii. Wizara imempata muwekezaji katika eneo la kihistoria la Fukuchani, ambaye ataliendesha na kulitangaza kimataifa eneo hilo. Vile vile, Wizara inaendelea na hatua za kuwahamasisha wadau wa Sekta binafsi kushirikiana na Serikali katika kuwekeza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini.

ix. Wizara kupitia Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, ilishiriki katika mkutano mkubwa nchini Senegal Aprili 2023 wa Viongozi na Maafisa wanaotekeleza na kusimamia Makumbusho ya Taifa. Mkutano ulilenga kuboresha uhusiano na kuainisha maeneo ya kushirikiana baina nchi tofauti na kubadilishana uzowefu. Tayari ushiriki wetu umezaa matunda na kuwavutia baadhi ya viongozi hao kuja kuitembelea Zanzibar na kuendelea na mazungumzo ya kushirikiana.

## CHANGAMOTO ZA WIZARA

10. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale licha ya kufanikiwa katika utekelezaji wa malengo na shughuli zake ilizojipangia, pia, inakabiliwa na changamoto mbali mbali miongoni mwao ni kama zifuatazo: -

i. Ukiukwaji wa masharti ya vibali kwa wamiliki wa nyumba za Mji Mkongwe ambao huzifanyia matengenezo majengo yao kinyume na vibali walivyoomba. Hali hii hupelekea kupoteza uhalisia wa majengo yaliyomo ndani ya Mji Mkongwe. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe

imekuwa ikichukua jitihada kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha ukarabati unafanyika kwa mujibu wa vibali vinavyotolewa pamoja na kuwaelimisha wakaazi na wadau wa Mji Mkongwe juu ya faida zinazopatikana katika kuuhifadhi na kuuendeleza mji huu wa kihistoria.

ii. Upungufu wa bajeti ya kukiendesha Kikosi cha Polisi Utalii na Diplomasia. Hali hii inapelekea kushindwa kwa kikosi hiki kufanya kazi kwa ufanisi. Katika kulitatua hili, Wizara inaendelea kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kikosi cha Utalii na Diplomasia na kuiomba Serikali kutenga bajeti ya kikosi hicho.

**a. Mapato yaliyokusanywa na Wizara kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2022-Machi 2023)**

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale katika mwaka wa fedha 2022/2023 imepangiwa kukusanya **Shilingi 7,200,000,000/=** hadi kufikia Machi 2023 imefanikiwa kukusanya **Shilingi 5,542,74P2,163/=** sawa na asilimia 76.98, fedha zote zilizoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1B)**.

**b. Fedha iliyopatikana kwa kipindi miezi tisa (Julai 2022-Machi 2023)**

12. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilikadiriwa kupata **Shilingi 17,289,100,000/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tano na Miradi ya Maendeleo ya Wizara. Kati ya hizo **Shilingi 6,092,001,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 3,697,099,000/=** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 7,500,000,000/=** kwa kazi za Maendeleo.

13. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilipata jumla ya **Shilingi 5,832,345,839.99/=** sawa na asilimia **33.7**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,718,188,264.99/=** zilipatikana kwa kazi za kawaida sawa na asilimia **41**. **Shilingi 4,114,157,575/= z**ilipatikana kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia **148** kwa upande wa kazi za miradi ya maendeleo zimepatikana **Shilingi 492,185,386/=** sawa na asilimia **7 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1A).**

## D. PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

14. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inatekeleza Malengo na Majukumu kwa kufuata Mfumo Maalumu wa Bajeti (Program Based Budget, PBB), ambapo Wizara inasimamia programu kuu tano na programu ndogo tatu.

### Programu Kuu za Wizara ni : -

i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.
ii. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii.
iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.
iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii.
v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

### Programu ndogo za Wizara ni: -

i. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara.
ii. Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

## E. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

15. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilipanga kutekeleza 'Programu ya Kuimarisha na Kuendeleza Maeneo ya Kihistoria' kwa kuyafanyia matengenezo maeneo yafuatayo:-

    i. Kuimarisha eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu – Pemba
    ii. Kuimarisha eneo la kihistoria la Mangapwani – Unguja
    iii. Kuimarisha Mahamamu ya Kidichi, Kizimbani, Forodhani na Hamamni – Unguja na
    iv. Kuimarisha eneo la Kihistoria la Maruhubi – Unguja

16. **Mheshimiwa Spika,** miradi ya kuimarisha maeneo ya kihistoria ipo katika hatua za ununuzi na za kuwapata wakandarasi. Kwa ujumla miradi hii imetengewa **Shilingi 7,500,000,000/=.** Kati ya fedha hizi, **Shilingi 500,000,000/=** zilitengwa kwa ajili ya kulipa deni la kampuni ya Kin Investiment Ltd na Shamjo Co Ltd ambao walifanya matengenezo ya eneo la kihistoria la Mkamandume awamu ya pili na eneo la kihistoria la Mvuleni.

## F. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI 2022-MACHI 2023.

17. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilipanga kutekeleza programu kuu tano kama ifuatavyo: -

    i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.
    ii. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii.
    iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.
    iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii.
    v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

## I. PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE.

18. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuwa na Mji Mkongwe na maeneo ya kihistoria yaliyohifadhiwa, kuimarishwa na kuendelezwa kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae. Matokeo ya muda mrefu ni kuyahifadhi, kuyalinda, kuyatangaza na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini pamoja na Uhifadhi wa Mji Mkongwe ili kubakia kuwa urithi wa kitaifa, kikanda na kimataifa.

19. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ya Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe inatekelezwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe.

20. **Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotolewa na programu hii ni Uhifadhi na Uendelezaji wa Makumbusho, Maeneo ya Kihistoria, Mambo ya Kale pamoja na Mji Mkongwe.

### UTEKELEZAJI HALISI

21. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imeratibu Mkutano wa Kimataifa wa Wanaakiolojia kutoka nchi za Afrika (Pan-African Archaelogical Association Conference) pamoja na mataifa mengine. Mkutano huo ulifanyika katika ukumbi wa Chuo cha Utalii Maruhubi, ambapo umehudhuriwa na washiriki wapatao 300. Mada mbali mbali zinazohusu Makumbusho na Mambo ya Kale zimewasilishwa na kujadiliwa. Mkutano huo umetoa fursa kwa Wanaakiolojia wa Zanzibar kutambua mambo mengi kuhusiana na tasnia yao. Kufanyika kwa mkutano huo nchini kumeleta mafanikio ya kuyatangaza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini.

22. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuendelea kulinda na kuhifadhi vitu vya kale vilivyopo nchini, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imekutana na wafanyabiashara wanaojishughulisha na uuzaji wa vitu vya kale kwa wageni. Lengo la mkutano huo ni kuwaelezea

umuhimu wa kulinda na kuhifadhi vitu vya kale vilivyopo nchini, ikiwemo taratibu za uuzaji na ununuaji, taratibu za usafirishaji pamoja na uingiaji wa mikataba ya kimataifa inayohusu vitu vya kale. Wafanyabiashara hao wameridhia kushirikiana na Serikali katika kulinda na kuhifadhi vitu vya kale vilivyopo nchini kwa lengo la kuendeleza historia halisi kwa faida ya vizazi vya sasa na vya baadae.

23. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imekutana na wadau wa Makumbusho na Mambo ya Kale wa Unguja na Pemba kwa lengo la kuwasilisha na kujadili Rasimu ya Mswaada wa Sheria ya Usimamizi ya Mamlaka ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Rasimu hii inalenga kuifuta Sheria ya Mambo ya Kale namba 11 ya mwaka 2002 inayotumika hivi sasa. Rasimu hii kwa sasa ipo katika hatua za kuwasilishwa katika vikao vya Makatibu Wakuu kwa lengo la kujadiliwa.

24. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuhakikisha elimu ya Makumbusho inawafikia wananchi kwa wepesi zaidi, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imefanya ziara za uhamasishaji katika skuli za Chanjamjawiri na Shamiani kisiwani Pemba. Pia ziara kama hizo zimefanyika katika Skuli ya Ukongoroni na Charawe kwa Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja. Ziara hizo zimewakutanisha walimu na wanafunzi na kuwaelimisha kuhusu dhana ya Makumbusho na Mambo ya Kale pamoja na dhana ya Utalii kwa Wote.

25. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho Mambo ya Kale imekamilisha upatikanaji wa hatimiliki za eneo la Msuka Mjini na Ngome Kongwe iliopo Chake Chake, Pemba. Vile vile, kwa upande wa Unguja maeneo yaliyopatiwa hatimiliki ni Hamam la Kidichi pamoja na Nyumba ya Kihistoria iliyopo Mwera. Pia, Idara imeyafanyia matengenezo mabango matano ya maelezo yaliyopo katika eneo la kihistoria la Chuini, Mangapwani, Msikiti wa Kizimkazi na Pango la Kuumbi kwa Unguja. Aidha, kwa upande wa Pemba ni bango la Pango la Kijiji.

26. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kutafuta na kupata taarifa za uhakika za maeneo mbali mbali ya kihistoria nchini, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imefanya tafiti za masimulizi ya Utumwa huko Dongoni, Shehia ya Kilindi Pemba. Baada ya kukamilika kwa tafiti hizi wataalamu wa Makumbusho huyahifadhi maelezo hayo kwa faida ya jamii.

27. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Idara imeandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 17 kupitia Redio na TV. Mfano Alfalah TV Online vipindi viwili, Zanzibar Cable vipindi viwili, Furaha FM vipindi sita, ZBC TV vipindi vitano, TBC TV kipindi kimoja na Isles Blog kipindi kimoja. Pia, Idara imepokea jumla ya wageni 11,671 ambao wametembelea maeneo na sehemu za kihistoria zilizopo Unguja na Pemba. Kati ya hao, wenyeji walikuwa 1,189 na watoto 40. Wageni watu wazima 1,756 na watoto 30, wanafunzi 8,641 kutoka Zanzibar na wageni maalumu 12 walitembelea maeneo ya kihistoria.

28. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imeendelea kuadhimisha Siku ya Dkt. Livingstone, ambae ni mvumbuzi na mmishionari maarufu aliyewahi kuishi hapa Zanzibar na kuacha historia kubwa ambayo imekuwa ni sehemu ya kivutio kwa wageni wanaoingia nchini. Siku ya Dkt. Livingstone huadhimishwa kila ifikapo **tarehe 19 Machi** ya kila mwaka, ambapo kwa mwaka huu shughuli zilizofanyika ni kufanya matembezi katika maeneo yote yenye kumbukumbu za mvumbuzi huyo, kwa lengo la kuendelea kuitunza historia hiyo. Matembezi hayo yamewashirikisha watembeza watalii, vijana wa Chama cha Mapinduzi, wanafunzi wa baadhi ya Skuli za Serikali na Binafsi pamoja na Dayosisi ya Kanisa la Anglikana Zanzibar.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuweka mazingira mazuri ya kazi pamoja na kuwa na wafanyakazi walio bora, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi watano katika ngazi za Shahada ya Rasilimali Watu wafanyakazi wawili, Stashahada ya Uhusiano wa Kimataifa mfanyakazi mmoja, Astashahada ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wafanyakazi

wawili. Aidha Idara imewapatia wafanyakazi tisa mafunzo ya muda mfupi, wakiwemo wafanyakazi wawili mafunzo ya Uhifadhi Taarifa za Maeneo ya Kihistoria Kielektroniki, wafanyakazi wawili Uhifadhi wa Kumbukumbu, wafanyakazi wanne mafunzo ya 'Graghic Design' na mfanyakazi mmoja mafunzo ya udereva.

30. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuhakikisha jengo la Beit el Ajaib linarudi katika uhalisia wake, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe imeshiriki katika makabidhiano ya jengo hilo kwa Mkandarasi ambaye ni **'Nandhra Engineering and Construction Ltd'** kutoka Tanzania Bara. Makabidhiano hayo yamefanyika mnamo **tarehe 19/03/2023** na kuwashirikisha wajumbe kutoka Serikali ya Ufalme ya Oman ambao ndio wafadhili wa matengenezo hayo. Shughuli hii imekuja baada ya kukamilika kitendo cha utiaji wa saini kilichofanyika nchini Oman mnamo **tarehe 13/03/2023.** Ujenzi huu unaanza **tarehe 19/06/2023** na kutarajiwa kukamilika mwaka 2026 kwa gharama za Dola za kimarekani **21,075,527.17/=.**

31. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imefanya kazi ya kulihami jengo la Kasri la Wananchi la Forodhani kwa kuliwekea vizuizi, kutengeneza kingo za maji na paa, kuziba nyufa zilizoashiria hatari ndani ya jengo na kufanya uchunguzi wa udongo (soil investigation) ili kuweza kujiandaa na matengenezo makubwa. Aidha, Mamlaka imeipitia na kuitolea maoni ripoti ya mwanzo ya hali ya jengo na 'Concept Design' zilizowasilishwa na Mshauri Elekezi, 'GMP Consulting Engineering', ambae ameshawasilisha ripoti ya pili 'Preliminary Design Report' kwa ajili ya kuipitia na kuitolea maoni.

32. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imesimamia na kutoa ushauri wa kitaalamu katika ujenzi wa Soko la Samaki la Malindi lililojengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Japan na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, maduka ya Darajani (Darajani Souk) yanayomilikiwa na Chama cha Mapinduzi na kujengwa na Kampuni ya Simba Developers Ltd. Kwa sasa ujenzi wote huo umekamilika na tayari maeneo hayo yanatumika kwa shughuli za kijamii. Pia, Mamlaka imesimamia ukarabati wa Soko la Darajani.

33. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuimarisha maeneo yaliyomo ndani ya Mji Mkongwe, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe imeyatengeneza Makaburi ya Mkunazini, Bustani ya Forodhani, kujenga kwa kiwango cha lami barabara na maegesho yaliyopo eneo la Msikiti wa Forodhani, kuanzisha sehemu maalumu kwa ajili ya wachoraji wa picha wa Mji Mkongwe katika njia iliyopo baina ya Hoteli ya Park Hyatt na Tembo 'Painting Corridor' ili kuondosha wachoraji holela ndani ya Mji Mkongwe. Aidha, Mamlaka imerejesha taa zilizokosekana kwa muda mrefu katika mitaa ya Mji Mkongwe, kupaka rangi majengo ya njiani, kuweka sawa nyaya na bomba za maji pamoja na kusafisha na kutoa nyavu katika Bwawa la Bwawani. Juhudi hizi zinafanyika makusudi kwa lengo la kuupa hadhi Mji wetu ili uendane na miji mengine ya kimataifa.

34. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha wananchi wa maeneo ya Mji Mkongwe wanapata elimu ya kutosha juu ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe, imetoa elimu ya Kanuni za Uhifadhi Mji Mkongwe kwa wananchi wa Shehia ya Shangani. Elimu hii itaendelea kutolewa kwa Shehia zote za Mji Mkongwe. Aidha, Mamlaka imetoa vibali 220 kwa kazi za matengenezo ya nyumba zilizomo ndani ya Mji Mkongwe. Vibali hivyo vimehusisha ujenzi wa nyumba mpya pamoja na matengenezo ya nyumba kongwe.

35. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi kwa wafanyakazi wake, Mamlaka imegharamia upatikanaji wa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 13 katika fani tofauti zikiwemo uhandisi mfanyakazi mmoja, Ofisi Mtandao wafanyakazi watano, Usimamizi wa Taarifa, Kumbukumbu na Nyaraka za Fedha mfanyakazi mmoja, Mpango Mkakati mfanyakazi mmoja, Usalama wa Kimtandao wafanyakazi wawili na mafunzo ya kuwajengea uwezo Makatibu Mahsusi na Watunza Kumbukumbu wafanyakazi watatu. Aidha, Mamlaka imegharamia safari za kikazi za Dar es Salaam, Arusha na Ufaransa kwa mfanyakazi mmoja kwenda kuwasilisha na kujadiliana kuhusu michoro ya mradi wa maegesho (parking) wa Malindi unaotekelezwa na ZSSF. Kukamilika kwa mradi huu kutaondoa changamoto ya maegesho ya magari katika eneo la Mjini.

36. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wa Mji Mkongwe imefanya maadhimisho ya Siku ya Mji Mkongwe kwa mwaka 2022 ambayo hufanyika kila ifakapo **tarehe 02 Disemba** ya kila mwaka. Kauli Mbiu ya mwaka huu ilikuwa **'Tuuhifadhi Mji Mkongwe kwa Vizazi vya Sasa na Vijavyo'**. Maadhimisho hayo hufanyika kwa lengo la kutambua thamani ya Kipekee ya Mji Mkongwe Kitaifa na Kimataifa pamoja na kuelimisha jamii juu ya uhifadhi na usimamizi wa Mji Mkongwe. Maadhimisho hayo yamehudhuriwa na Jumuiya mbali mbali za Uhifadhi za ndani pamoja na kuwepo kwa maonesho yenye kutoa elimu juu ya uhifadhi wa majengo ya Mji Mkongwe. Mamlaka imekamilisha utayarishaji wa Kanuni za Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ambazo zimenza kutumika.

37. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 9,990,830,000/=** hadi kufikia Machi 2023 imefanikiwa kupata **Shilingi 2,338,523,053.45/=** sawa na asilimia **23**. **Shilingi 1,018,750,000/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, hadi kufika Machi 2023 S**hilingi 279,532,267.45/=** zilipatikana sawa na asilimia **27** na **Shilingi 1,472,080,000/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara hadi kufikia Machi 2023 imefanikiwa kupata **Shilingi 1,566,805,400/=** sawa na asilimia **106** ya makadirio. Vile vile, program hii ilipangiwa **Shilingi 7,500,000,000/=** Kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maendeleo hadi kufikia machi 2023 imepata **Shilingi 492,185,386/=** sawa na asilimia 7. Aidha, Programu ilitakiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 950,000,000/=**, hadi kufikia Machi 2023 imekusanya jumla ya **Shilingi 415,303,775/=** sawa na asilimia **44**. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C na 1D)**

## II. PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

38. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuratibu na kusimamia shughuli za utalii nchini. Matokeo ya muda mrefu ni kuwa na utalii endelevu na wenye tija kwa maslahi ya nchi na wananchi. Huduma zinazotolewa katika programu hii ni kusimamia utekelezaji

wa sera, sheria na mipango ya utalii. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Utalii.

## UTEKELEZAJI HALISI

39. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kukitangaza kisiwa cha Pemba kiutalii, Idara ya Utalii imefanya uzinduzi wa filamu ya **"THE ROYAL TOUR"** ambayo inaonesha fursa zilizopo za uwekezaji na kiutalii katika kisiwa hicho kwenye Kiwanja cha Gombani Chake-Chake, Pemba. Katika uzinduzi huo zaidi ya wananchi 200 kutoka maeneo mbali mbali ya Pemba walihudhuria. Vile vile, Idara imeshiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani ambayo hufanyika kila ifikapo tarehe 27 Septemba ya kila mwaka. Maadhimisho hayo yamewashirikisha makampuni mbali mbali ya watembeza watalii pamoja na kampuni za usafirishaji watalii.

40. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii imetoa mafunzo kwa watembeza watalii 65 katika maeneo ya mashamba ya viungo (Spice Farms), ambayo yamelenga kutoa elimu juu ya uoteshwaji wa baadhi ya miti ya viungo pamoja na ukarimu kwa wageni. Pia, Idara ya Utalii imefanya tathmini ya kuyaimarisha mashamba hayo kwa kuandaa michoro pamoja na Wazo la Mradi (Project Proposal). Kwa sasa, Idara inaendelea kuwasiliana na Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kuyaimarisha mashamba hayo, ili yaweze kuleta tija kwa wamiliki.

41. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua za kusimamia na kuimarisha usafi katika Maeneo na Vivutio vya Utalii nchini, Idara ya Utalii kwa kushirikiana na Kamati ya Utalii ya Wilaya ya Magharibi B, ilifanya usafi katika Kisiwa cha Kwale. Shughuli hiyo ilikwenda sambamba na kampeni ya upigaji vita ajira kwa watoto kwenye maeneo ya kitalii. Vile vile, Idara kwa kushirikiana na wadau wa Chama cha Mazoezi (ZABESA) imefanya usafi katika Kisiwa cha Changuu (Prison Island), kwa lengo la kuwavutia wageni wengi kuweza kutembelea Kisiwa hicho.

42. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuimarisha utoaji wa huduma kwa wageni wanoingia nchini, Idara ya Utalii imetoa mafunzo ya Ukarimu kwa kampuni zinazosimamia usalama wa wageni. Mafunzo hayo yamewashirikisha Polisi Utalii na Diplomasia pamoja na kampuni binafsi za ulinzi zilizopo nchini. Aidha, Idara imeendesha kampeni maalumu ya kuwahamasisha wananchi wa maeneo ya Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Kati kupitia Kamati za Utalii za Wilaya hizo pamoja na Masheha wa Shehia, kushiriki katika kuvitembelea Vivutio vya Utalii vilivyopo katika Wilaya zao. Kampeni hii imelenga kukuza Utalii wa Ndani na kufikia dhamira ya Utalii kwa Wote. Kadhalika, ninachukua fursa hii kuwahamasisha Wahishimiwa Wajumbe wa Baraza lako kuwa Mabalozi wetu wa kuwahamasisha wananchi katika maeneo mnayoyaongoza kuvitembelea Vivutio vya Utalii vilivyopo katika maeneo yenu.

43. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kubuni na kuvumbua vivutio vipya vya utalii nchini, Idara ya Utalii kwa upande wa Pemba kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo husika wamevumbua maeneo mapya sita ambayo ni Mto Furaha, Mji wa Kihistoria na Jamati la Wahindi Kengeja, Pango la Samaki, Majabali ya Katenga, Shamba la Viungo Wambaa na Gando. Kuongezeka kwa idadi ya vivutio hivyo nchini kutachochea kuongezeka kwa siku za ukaazi kwa wageni. Vile vile, Idara ya Utalii kwa kushirikiana na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), tawi la Pemba wamefanya ziara ya kuvitembelea vivutio vya utalii vya Msitu wa Ngezi pamoja na eneo la kihistoria la Mkamandume. Ziara hizo zimelenga kupata historia kamili za maeneo hayo pamoja na kutambua aina ya miti na wanyama wanaopatikana kwa wingi katika Msitu wa Ngezi.

44. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii imeandaa na kurusha hewani vipindi saba vya uelimisha jamii kuhusu utalii, ambavyo vimerushwa kupitia ZBC TV kipindi kimoja, ZBC Redio kipindi kimoja, Chuchu FM Redio kipindi kimoja, ZBC TV Pemba vipindi viwili na vipindi viwili Pemba Today Online. Pia, Idara imechapisha makala moja kupitia Gazeti la Zanzibar Leo inayohusu Utalii.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 401,360,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2023 imefanikiwa kupata **Shilingi 82,053,685.11/=** sawa na asilimia 20, jumla ya **Shilingi 244,870,000/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya Mishahara na hadi kufikia Machi 2023 imefanikiwa kupata **Shilingi 192,794,600/=** sawa na asilimia 78.7 **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C)**.

## III. PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII

46. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuongeza uelewa kwa wakaazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusu bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Programu inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

47. **Mheshimiwa Spika,** huduma inayotolewa katika programu hii ni kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi ili Zanzibar itambulike zaidi kuwa ni kituo bora cha utalii duniani.

### UTEKELEZAJI HALISI

48. **Mheshimiwa Spika**, katika kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi, Kamisheni ya utalii imeshiriki maonesho ya utalii ya kimataifa ya ITB (Internationale Tourismus Börse) - Berlin, maonesho ya wazi (Road show) katika nchini za Ujerumani, Uholanzi, Ubelgiji na Ufaransa. Aidha, Kamisheni imeshiriki katika ziara za viongozi katika nchi za Oman, Qatar na Saudia Arabia. Vile vile, katika kuhamasisha utalii wa ndani Kamisheni imeshiriki katika maonesho ya Swahili Expo (SITE) - Dar –es- salaam, Maonesho ya Wanawake na Vijana katika Biashara chini ya Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika – Dar es salaam, Maonesho ya Kili Karibu Fair – Arusha, Maonesho ya Kilimo - nane nane – Kizimbani, Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) - Dar es Salaam, Maonesho ya Biashara katika kuadhimisha miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar - Maisara na Tamasha la Kizimkazi.

49. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii imepokea, waandishi wa habari watatu kutoka Kampuni ya EBS ya nchini Korea ya Kusini ambao wamepiga picha katika maeneo mbali mbali ya utalii Unguja na Pemba na kuandaa makala 'documentary' ambazo zitaoneshwa katika televisheni na mitandao ya kijamii. Aidha, jumla ya watu mashuhuri watatu wameingia nchini na kuvitembelea vivutio mbali mbali vya utalii ambao ni: Muigizaji maarufu kutoka Hollywood – Marekani, Lupita Nyong'o na msanii mashuhuri wa Nashed duniani, Maher Zain na Sunj Dutt mwigizaji wa filamu kutoka nchini India. Aidha, wachezaji mpira wa miguu maarufu wakiwemo Samuel Et'oo, Ander Herera, Ibrahima Konate, na Stefen de Vrij walitembelea Zanzibar. Pia, Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na wadau wengine iliandaa Tanzania Football Summit, ambapo Kamisheni ilikutana na wachezaji soka maarufu duniani, wakiwemo Avram Grant na Khalilou Fadiga. Kupitia watu hawa Zanzibar itatangazwa kiutalii katika nchi zao na nchi nyengine duniani.

50. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha vivutio vya utalii vinatangazwa ipasavyo Kamisheni ya Utalii kupitia Mradi Shirikishi wa Ufufuaji wa Utalii Zanzibar 'Integrated Tourism Recovery and Resilience' unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) inaandaa 'web portal' ya Utalii ambayo itatengeneza jukwaa la utalii litakaloitangaza Zanzibar kidijitali. Aidha, kwa kupitia mradi huo na kwa kushirikiana na SMIDA imeandaa jukwaa la masoko kwa wajasiriamali wadogo wadogo na wakati kwa lengo la kuuza na kutangaza bidhaa zao kidigitali ili ziendane na thamani ya utalii. Kukamilika kwa kazi hiyo kutawawezesha wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati kutangaza bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

51. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na jitihada zinazochukuliwa na Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa utalii kuvitangaza vivutio vya utalii vya Zanzibar ndani na nje ya nchi, katika mwaka 2022 idadi ya watalii walioingia nchini imefikia 548,503. Idadi hii imepindukia watalii 538,264, walioingia nchini kwa mwaka 2019 kabla ya kuibuka kwa maradhi ya UVIKO 19,

ambapo idadi ya wageni ilishuka hadi kufikia 260,644 kwa mwaka 2020. Wizara inaendelea kufanya utafiti wa kuangalia wageni kutoka Tazania Bara ambao wanaingia Zanzibar

52. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/2023 program hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 650,616,500/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2023 imefanikiwa kupata **Shilingi 383,531,635/=** sawa na asilimia **59**. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C**).

## IV. PROGRAMU YA KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

53. **Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii na kuweka mazingira bora ya rasilimali katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii. Programu hii imeundwa na programu ndogo mbili ambazo ni:

   i. Utawala, Rasilimali Watu na Mipango
   ii. Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii

54. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala, Rasilimali Watu na Mipango inatekelezwa na Idara ya Rasilimali Watu, Mipango na Utawala.

### UTEKELEZAJI HALISI

55. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha upatikanaji wa taarifa za kutosha za watalii wanapoingia nchini Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Uhamiaji na Ofisi ya Taifa ya Takwimu wanaendelea na utafiti wa utokaji wa wageni (Visitors Exit Survey) kwa mwaka 2022, ambapo kwa sasa utafiti huo upo katika hatua za uandishi wa ripoti. Utafiti huo, utapelekea kufahamu baadhi ya viashiria muhimu vya upimaji wa ukuaji wa sekta ya utalii ikiwemo matumizi ya mtalii kwa siku pamoja na siku zao za ukaazi.

56. **Mheshimiwa Spika**, katika kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi, Kamisheni ya Utalii imegharamia safari za kikazi za ndani pamoja na vikao vya mashirikiano na taasisi za Tanzania Bara. Vile vile, Kamisheni ya Utalii imewapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 15 katika fani ya uongozi, utoaji wa huduma, utumiaji wa mifumo ya Serikali, mitandao ya kifedha, udhibiti wa wizi wa mitandao na Rasilimali Watu na Utalii Endelevu. Pia, wafanyakazi sita wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu kama ifuatavyo; wafanyakazi wawili Shahada ya Pili katika Uongozi wa Utalii, mfanyakazi mmoja Shahada ya kwanza ya Rasilimali Watu, mfanyakazi mmoja Shahada ya Pili Masoko na Uhusiano, mfanyakazi mmoja Shahada ya Pili ya Utawala na mfanyakazi mmoja masomo ya Cheti ya Uhifadhi wa Kumbukumbu.

57. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/2023 program hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,810,803,500/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2023, imefanikiwa kupata **Shilingi 370,472,338/=** sawa na asilimia 20, **shilingi 848,000,000/=** kwa ajili ya Mishahara na hadi kufikia Machi 2023 imefanikiwa kupata **Shilingi 1,112,672,680/=** sawa na asilimia **131** na kutakiwa kukusanya jumla ya **shilingi 6,200,000,000/=** na hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **shilingi 5,008,761,030.28/=** zimekusanywa sawa na asilimia **81 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C na 1D)**.

58. **Mheshimiwa Spika**, programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii inatekelezwa na Idara ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii yenye jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya utalii nchini.

## UTEKELEZAJI HALISI

59. **Mheshimiwa Spika**, Kamisheni ya Utalii imeendelea kufanya ukaguzi wa miradi ya biashara za utalii ili kujiridhisha na huduma zinazotolewa pamoja na kubaini miradi inayofanya biashara kinyume cha Sheria ya Utalii. Kazi hiyo imefanyika katika mikoa yote ya Zanzibar. Katika ukaguzi huo, jumla ya miradi ya utalii

348 imekaguliwa, ambayo imejumuisha hoteli, mikahawa, michezo ya baharini na kampuni za kuandaa misafara ya watalii. Pamoja na mambo mengine ukaguzi huo pia uliangalia idadi ya vyumba na wafanyakazi, huduma zinazotolewa pamoja na kutoa ushauri wa uendeshaji bora wa biashara zao. Aidha, Kamisheni imefanya ukaguzi wa vibali kwa gari zinazochukua watalii katika Mikoa yote ya Zanzibar.

60. **Mheshimiwa Spika**, Kamisheni imeendesha mafunzo kwa wajasiramali 384 wanaojishughulisha na biashara ya utalii katika maeneo ya Pwani Mchangani, Matemwe, Nungwi na Kendwa. Lengo la mafunzo hayo ni kuwaelimisha wananchi juu ya fursa zinazopatikana katika sekta ya utalii pamoja na kufanya shughuli zao kwa kufuata sheria na kanuni za nchi. Aidha, Jumla ya wananchi 25 kutoka Wilaya ya Micheweni walipatiwa mafunzo juu ya umuhimu wa utalii wa kihistoria.

61. **Mheshimiwa Spika**, katika kuwaelimisha wananchi juu ya fursa zinazopatikana katika sekta ya utalii na kuwa na utalii endelevu unaochochea uchumi wa bluu, Kamisheni ya Utalii imeandaa na kurusha vipindi 50 kupitia Redio na Televisheni zifuatazo: ZBC Redio vipindi 21, ZBC TV vipindi vitano, ZC TV vipindi vitano, Bahari FM vipindi viwili, Furaha FM vipindi 12, DW TV kipindi kimoja, redio ya Jamii Micheweni vipindi viwili na Redio ya Jamii Mkoani vipindi viwili.

62. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ulinzi na usalama wa wageni na mali zao pamoja na sekta ya utalii kiujumla, Kamisheni ya Utalii kupitia Kikosi cha Polisi Utalii na Diplomasia wamefanya doria katika maeneo ya utalii kama vile Mji Mkongwe, Uwanja wa Ndege, Bandarini, Mizingani, Forodhani, Posta Kongwe, Gizenga, Mkunazini, Marikiti ya Darajani, Makunduchi, Jambiani, Paje, Bwejuu, Michamvi, Kizimkazi, Pongwe, Uroa, Matemwe, Pwani Mchangani, Nungwi, Kiwengwa na Kendwa. Kufanyika kwa doria hizo kumepunguza vitendo vya uhalifu katika maeneo hayo. Aidha, katika kuongeza ufanisi na uweledi, jumla ya Askari 120 wa kikosi

cha Polisi Utalii na Diplomasia wamepatiwa mafunzo juu ya ulinzi na usalama wa watalii na mali zao kwa ufadhili wa Ubalozi wa Uingereza nchini. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inatarajia kuzindua kikosi hiki rasmi kwa upande wa Pemba.

63. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/2023 program ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 564,180,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2023 imefanikiwa kupata **shilingi 126,251,420/=** sawa na asilimia **22**. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C)**.

## V. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

64. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii imeundwa na programu ndogo tatu ambazo ni:

i. Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Utalii na Mambo ya Kale
ii. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

65. **Mheshimiwa Spika**, programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Utalii na Mambo ya Kale inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

66. **Mheshimiwa Spika**, huduma zinazotolewa katika programu ndogo ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi, utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi pamoja na mpango wa manunuzi.

## UTEKELEZAJI HALISI

67. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kuwajengea uwezo wafanyakazi wake 14 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu katika fani na ngazi tofauti. **(Tafadhali Angalia Kiambatanisho nambari 2)**. Aidha, wafanyakazi 15 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya Zanzibar. Kadhalika, wafanyakazi 52 wamepatiwa mafunzo ya ndani ya Wizara juu ya Kuimarisha Utendaji kazi wa Divisheni ya Kumbukumbu, Matumizi ya Mfumo wa Manunuzi ya Mtandao na Ofisi Mtandao, Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, Sheria na Kanuni za Fedha pamoja na Sheria na Kanuni za Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali. Pia wafanyakazi 37 wamepatiwa semina juu ya kuzuia na kupambana na rushwa na uhujumu uchumi katika maeneo ya kazi pamoja na Afya na Usalama katika mahala pa kazi.

68. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imesimamia ufanyaji wa tathmini ya utendaji kazi wa wafanyakazi wake 319 Unguja na Pemba na kujiridhisha na utendaji wao. Vile vile, Viongozi wa Wizara waliweza kufuatilia utendaji kazi Pemba na kushiriki katika vikao kazi na mikutano Tanzania Bara. Pia, Idara imeratibu vikao vya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi ya Wizara kwa ajili ya kujadili Sera, Kanuni, Sheria, Miongozo, Miradi ya Maendeleo na mambo mbali mbali yanayohusu Wizara.

69. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mashirikiano baina ya Wizara, Taasisi na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, Wizara imefanya jumla ya vikao 39 na Wadau wa Utalii na Mambo ya Kale wa ndani na nje ya nchi na kujadili maendeleo ya sekta. Kadhalika, katika kuimarisha utekelezaji wa shughuli zake, Wizara imeshiriki katika Mkutano wa Kimataifa wa UNESCO uliofanyika nchini Urusi na Kongamano la Kimataifa la Utalii nchini Saudi Arabia, Ziara ya Kikazi na kushuhudia Utiaji saini Mkataba wa Ujenzi wa Jengo la Beit Al Ajaib nchini Oman. Wizara pia, imepokea wageni 24 kutoka mataifa mbali mbali na Mashirika ya Kimataifa kwa lengo la kuimarisha uhusiano mwema na mashirikiano ya utekelezaji wa shughuli za Wizara na

nchi za Oman, China, Kenya, Saudi Arabia, India, Urusi, USA, Brazil, Ufaransa, Italia na Qatar pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo UNESCO, UNDP na UNICEF.

70. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 900,000,000/= kwa kazi za kawaida, **Shilingi 656,368,000/=** kwa ajili ya Mishahara hadi kufikia Machi 2023 imefanikiwa kupata **Shilingi 314,608,628.6/=** kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 34.96 na kupata **Shilingi 746,733,210/=** kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia **113.77**. **(Tafadhali angalia kiambatisho nambari 1C)**.

71. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya kuratibu na kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kufuatilia na kutathmini Mipango, Sera, Tafiti na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

72. **Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa sera na tafiti, kuandaa na kuwasilisha bajeti ya Wizara, kuandaa na kusimamia mipango na miradi ya maendeleo ya Wizara.

## UTEKELEZAJI HALISI

73. **Mheshimiwa Spika,** Idara Mipango, Sera na Utafiti imekamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Makumbusho na Mambo Kale pamoja na Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo. Kukamilika kwa Sera hii kutaiwezesha Idara Makumbusho na Mambo ya Kale kuwa na nguvu zaidi katika kuyalinda, kuyahifadhi, kuyasimamia na kuyaimarisha maeneo na vitu vya kale. Aidha, Idara imekamilisha rasimu ya Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Makumbusho na Mambo ya Kale na ipo kwenye hatua za kuwasilishwa kwa Kamati ya Makatibu Wakuu. Pia, Idara imeandaa na kuwasilisha kwa Wadau wa Utalii wa Unguja na Pemba Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Utalii ya Mwaka 2017, kwa lengo la maandalizi ya kufanya Mapitio ya Sera hiyo ya Utalii, ambayo inatarajiwa kufanyiwa mapitio na kuandaa Mpango wa Utekelezaji katika mwaka wa fedha 2023/2024,

ili kwenda sambamba na mahitaji ya Sekta ya Utalii. Pia Idara imekamilisha hatua za awali za Utafiti wa Uwezo wa Zanzibar wa Kuhimili Watalii (Zanzibar Tourism Carrying Capacity). Tayari Wizara imekamilisha taratibu za zabuni na kumpata Mshauri Elekezi wa utafiti huo ambao unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2023.

74. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kusimamia utekelezaji wa miradi ya eneo la kihistoria la Chwaka Tumbe, Pango la Watoro na Pango la Kijiji, Makumbusho ya Amani na Viumbe Hai na ujenzi wa jengo jipya la Wizara, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeratibu zoezi zima la kukabidhiwa kwa Miradi ya Maendeleo ya mwaka wa fedha 2021/2022. Kukamilika kwa miradi hii ya kihistoria kunaongeza idadi ya vivutio vya utalii vilivyoimarishwa nchini. Aidha, Idara imeratibu utekelezaji wa miradi ya Wizara ya mwaka wa fedha 2022/2023, ambayo ni eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu, Mangapwani, Maruhubi pamoja na Mahamamu ya Forodhani, Kidichi, Kizimbani na Hamamni. Tayari miradi ya Ras Mkumbuu Pemba na Mangapwani imeshakabidhiwa kwa Wakandarasi. Miradi iliobakia ipo kwenye hatua za manunuzi.

75. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mahusiano na mashirikiano ya kiutendaji baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeratibu vikao vya ushirikiano kwa Sekta ya Utalii, Mambo ya Kale na Maliasili vilivyowashirikisha Wizara ya Maliasili na Utalii (SMT), Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale (SMZ) na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo (SMZ). Vikao hivyo vilifanyika Jijini Dodoma mwezi Disemba na kujadili masuala mbali mbali ya Muungano na yasiyo ya Muungano ambayo yatasaidia katika kukuza sekta hizi kwa manufaa ya Taifa. Vikao vya ufuatialiaji wa maazimio baina ya pande mbili za Muungano vinaendelea.

76. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imetayarisha na kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Malengo na Shughuli za Wizara kwa Tume ya Mipango, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais,

Ofisi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Kisiwandui pamoja na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Aidha, Idara imefanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Malengo na Shughuli zinazotekelezwa na Idara na Taasisi za Wizara.

77. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuimarisha utendaji kazi kwa wafanyakazi wake, Idara inagharamia masomo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wake wawili, mmoja anayesomea Shahada ya Pili ya Miradi na mfanyakazi mwengine anaesoma Shahada ya Pili ya masuala ya Sera. Pia, Idara imegharamia mafunzo ya muda mfupi ya miradi kwa mfanyakazi wake mmoja.

78. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/2023, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 300,000,000/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 109,741,080** kwa ajili ya Mishahara na hadi kufikia Machi 2023 imefanikiwa kupata **Shilingi 102,251,968.66/=** kwa kazi za kawaida sawa na asilimia **34** na **Shilingi 126,021,130/=** kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia **114.8 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C)**.

79. **Mheshimiwa Spika**, programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba.

80. **Mheshimiwa Spika**, huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa Sera, Tafiti na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu Pemba, kuratibu Miradi ya Maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

## UTEKELEZAJI HALISI

81. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imeratibu mapitio ya Sera ya Utalii ya mwaka 2017, Rasimu ya Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Makumbusho na Mambo ya Kale Zanzibar, pamoja na Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Makumbusho na Urithi wa Mambo ya Kale kwa wadau waliopo kisiwani Pemba. Aidha, Ofisi Kuu Pemba

imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli na miradi ya Wizara na kuratibu zoezi la makabidhiano ya miradi ya mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni Miradi ya eneo la kihistoria la Chwaka Tumbe, Pango la Kijiji na Pango la Watoro pamoja na kukabidhi eneo la Ras Mkumbuu kwa Mkandarasi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

82. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imeratibu zoezi la uchukuaji wa filamu katika vivutio vya utalii vya Chwaka Tumbe, Pango la Watoro, Pango la Kijiji na Mnara wa Kigomasha. Lengo la filamu hiyo ni kuhamasisha jamii pamoja na kampuni za watalii kuweza kuwatembeza wageni katika maeneo hayo. Pia, katika hatua za kukikuza kisiwa cha Pemba katika nyanja ya utalii, Ofisi Kuu Pemba imeratibu Tamasha la Siku ya Utalii Duniani lililofanyika tarehe 27/09/2022 katika Kiwanja cha Watoto cha Tibirinzi.

83. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imegharamia upatikanaji wa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wawili, mmoja anaesomea Utunzaji wa Kumbukumbu katika ngazi ya Diploma na mfanyakazi mwengine anaesomea Usimamizi na Upangaji wa Miradi katika ngazi ya Shahada ya Pili. Vile vile, Ofisi Kuu Pemba imegharamia upatikanaji wa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi saba wa Divisheni ya Mipango, Sera na Utafiti, Divisheni ya Kumbukumbu, Divisheni ya Utumishi pamoja na Kitengo cha Manunuzi na Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

84. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 443,563,400/=**, kwa ajili ya kazi za kawaida, **Shilingi 366,040,495/=** kwa ajili ya Mishahara, hadi kufikia Machi 2023 imefanikiwa kupata **Shilingi 94,421,418 /=** kwa kazi za kawaida sawa na asilimia **21** na **Shilingi 369,130,555/=** kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia 101. Programu ndogo hii imetakiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 50,000,000/=**, hadi kufikia Machi 2023, jumla ya **Shilingi 2,536,215/=** zimekusanywa sawa na asilimia **5**. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C na 1D)**.

## G. VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024.

85. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na mambo mengi imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuendelea kuitangaza Zanzibar Kimataifa kwa lengo la kutafuta masoko mapya yatakayochangia kukuza utalii wa nchi.
ii. Kuandaa mfumo wa kidijitali katika kuboresha huduma za Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale
iii. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa jengo la Beit el Ajaib ili liweze kurudi katika hali yake ya awali.
iv. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria yakiwemo, eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu, eneo la kihistoria la Mangapwani, eneo la kihistoria la Maruhubi, Mahamamu ya Kidichi, Hamamni, Forodhani na Kizimbani pamoja na kuweka maonesho katika majengo yaliyokamilika ujenzi wake kama vile Bungi kwa Bikhole, Mwinyi Mkuu Dunga, Fukuchani, Mvuleni, Mkamandume, Chwaka Tumbe, Pango la Kijiji na Makumbusho ya Amani na Makumbusho ya Viumbe Hai.

## H. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

86. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, Wizara ya Utalii, na Mambo ya Kale imepangiwa jumla ya **Shilingi 13,984,900,000/=**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,858,000,000/=** kwa matumizi ya kawaida, **Shilingi 4,126,900,000/=** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 7,000,000,000/=** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, Wizara imepangiwa kukusanya mapato yanayokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali **Shilingi 1,000,000,000/=. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1E, 1F, 1G)**.

87. **Mheshimiwa Spika,** katika fedha za matumizi ya kawaida ambazo ni **Shilingi 6,984,900,000/=**, **Shilingi 3,289,700,000/=** ni mishahara kwa taasisi za Wizara zisizo za ruzuku, **Shilingi 2,545,000,000/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa taasisi za Wizara zisizo za ruzuku. Aidha, **Shilingi 837,200,000/=** kwa ajili ya mishahara kwa taasisi ya Wizara ya ruzuku na **Shilingi 313,000,000/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa taasisi za Wizara za ruzuku. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F)**.

88. **Mheshimiwa Spika**, katika fedha za miradi ya maendeleo **Shilingi 7,000,000,000/=** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F)**.

89. **Mheshimiwa Spika**, naomba kukuarifu wewe pamoja na Wajumbe wa Baraza lako kwamba, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Kamisheni ya Utalii inatarajiwa kuanza rasmi utaratibu wa kutumia fedha inayotokana na Makusanyo yake kutoka vyanzo tofauti. Jumla ya fedha inayotarajiwa kukusanywa ni **Shilingi 10,295,888,120/=**, kati ya hizo **Shilingi 4,800,000,000/=** zitaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina, **Shilingi 1,725,888,120/=** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 3,770,000,000/=** kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kawaida.

## I. KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU (PROGRAM BASED BUDGET - PBB) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

90. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imepangiwa kutumia jumla ya **shilingi 13,984,900,000/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tano ambazo ni: -

i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe. (**Shilingi 10,085,599,000/=**).

ii. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii. (**Shilingi 658,677,000/=**).

iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii. (**Shilingi 890,410,000/=**).

iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii. (**Shilingi 4,605,478,120/=**).

v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika sekta ya Utalii na Mambo ya Kale. (**Shilingi 3,240,624,000/=**). (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F**)

**Programu ya Kwanza: Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe**

**91. Mheshimiwa Spika**, programu hii inatekelezwa na Idara ya Makumbusho pamoja na Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe. Programu hii ina jukumu la kuhakikisha kwamba maeneo ya Kihistoria na Mambo ya Kale yanaendelezwa kwa kuhifadhiwa, kulindwa na kutangazwa pamoja na kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe ili uendelee kubaki kuwa urithi wa dunia kwa kutoa faida kwa kizazi cha sasa na baadae. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni Kuyaimarisha Maeneo ya Kihistoria pamoja na Kuuendeleza Mji Mkongwe. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 10,085,599,000/=**.

**92. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kufanya Utafiti wa Akiolojia
ii. Kuanzisha Makumbusho katika maeneo ya kihistoria ya Bi Khole, Makumbusho ya Amani, Mkamandume na Pango la Kijiji.

iii. Kuanzisha kituo cha kujifunzia mambo ya Makumbusho (Study Center) Dunga
iv. Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu na kusimamia Uhifadhi wa Majengo na maeneo ya Mji Mkongwe.
v. Kuimarisha maeneo, majengo na miundombinu ndani ya Mji Mkongwe.
vi. Kutoa taaluma kwa taasisi za Serikali, binafsi na jamii kwa ujumla kuhusiana na umuhimu wa kuhifadhi na kuutunza Mji Mkongwe.
vii. Kuutangaza Mji Mkongwe kitaifa na kimataifa.
viii. Kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.

93. **Mheshimiwa Spika**, ili programu hii iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, naiomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **shilingi 963,000,000/=** kwa kazi za kawaida, **shilingi 2,122,599,000/=** kwa ajili ya Mishahara, **shilingi 7,000,000,000/=** kwa kazi za Maendeleo. Pia, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuiidhinishe Makusanyo ya Programu hii ya **shilingi 950,000,000/=**.

**Programu ya Pili: Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii.**

94. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii inatekelezwa na Idara ya Utalii. Jukumu la msingi katika programu hii ni Kusimamia na Kuratibu shughuli za Utalii pamoja na Kuwahamasisha Wananchi juu ya Dhana ya Utalii kwa Wote. Matokeo ya muda mrefu ni kuwa na utalii wenye kuleta manufaa kwa wananchi. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Uratibu na Uendelezaji wa shughuli za Utalii.

95. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuibua na kuviendeleza vivutio vipya vya utalii nchini.

ii. Kuzishirikisha Kamati za Utalii za Wilaya pamoja na wananchi katika kuendeleza dhana ya Utalii kwa Wote.
iii. Kuandaa na kutoa mafunzo kwa watembeza watalii juu ya ubora wa utekelezaji wa kazi zao.
iv. Kuwakutanisha wajasiriamali na wamikili wa mahoteli ili kupata masoko kwa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali hao.

96. **Mheshimiwa Spika**, ili programu hii iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya Shilingi 411,800,000/= kwa kazi za kawaida na Shilingi 246,877,000/= kwa ajili ya Mishahara.

**Programu ya Tatu: Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.**

97. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuongeza uelewa kwa wakazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusu bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Programu inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

98. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo : -

i. Kuandaa na kushiriki maonesho, mikutano na makongamano ya utalii ya kitaifa na kimataifa ili kuvutia wageni kuvitembelea vivutio vya utalii vya Zanzibar.

ii. Kuwaalika waandishi wa habari za utalii wa kimataifa, wamiliki wa mitandao ya kijamii na watu mashuhuri ili Zanzibar ipate fursa ya kutangazwa kupitia watu hawa kwa gharama nafuu.

iii. Kuongeza bidhaa za Utalii kwa kuandaa Matamasha ya mchezo kama vile Marathon, Triathon, kite surfing na Pemba Tourisport Bonanza.

99. **Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2023/2024, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha makusanyo yatakayotumiwa na programu hii ambayo ni jumla ya Shilingi 890,410,000/= kwa kazi za kawaida.

**Programu ya Nne: Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii**.

100. **Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii na kuweka mazingira bora na rasilimali watu katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii. Programu hii itatekelezwa na Kamisheni ya Utalii, ambayo itakuwa na programu ndogo mbili nazo ni:-

i. Utawala, Rasilimali Watu na Mipango
ii. Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii

101. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala, Rasilimali Watu na Mipango, inatekelezwa na Idara ya Rasilimali Watu, Mipango na Utawala. Programu ndogo hii ina lengo la kupanga na kuimarisha uwezo wa Kamisheni ili iweze kutekeleza majukumu yake.

102. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024 programu ndogo ya Utawala, Rasilimali Watu na Mipango inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kufanya tafiti wa utokaji wa wageni ili kufahamu baadhi ya viashiria muhimu vya upimaji wa ukuaji wa sekta ya utalii ikiwemo matumizi ya mtalii kwa siku.
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu

iii. Kuandaa na kuendesha vikao vya Makamishna na Wadau wa Utalii
iv. Kufanya tathmini na kufuatilia shughuli za Kamishemi ya Utalii na Miradi ya Maendeleo.
v. Kufanya Tathmini ya Rasilimali Watu katika Kamisheni ya Utalii

103. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2023/2024, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo yatakayotumiwa na programu ndogo hii, ambayo ni **Shilingi 1,885,985,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 1,725,888,120/=** kwa ajili ya mishahara. Pia, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo ya Programu hii ya S**hilingi 4,800,000,000/=** zitakazoingia Mfuko Mkuu wa Hazina.

104. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu na Shughuli za Utalii, inatekelezwa na Idara ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii. Programu ndogo hii ina lengo la kusimamia na kuratibu maendeleo ya Utalii nchini kwa kushajihisha uwekezaji vitega uchumi katika sekta ya Utalii Zanzibar.

105. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024 programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kukagua na kufuatilia miradi ya utalii ili kuhakiki huduma zinazotolewa.
ii. Kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu sekta ya Utalii pamoja na fursa zinazopatikana kwa kutumia radio, televisheni na makongamano.
iii. Kuandaa mafunzo kwa maofisa watakaofanya kazi ya kuweka viwango vya madaraja kwa bidhaa za utalii kwa vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.
iv. Kuainisha hoteli na mikahawa ambayo itafanyiwa

zoezi la kuwekewa viwango vya madaraja kwa huduma zinazotolewa.

**106. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2023/2024, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo yatakayotumiwa na Programu ndogo hii ya **Shilingi 993,605,000/=** kwa kazi za kawaida.

## Programu ya Tano: Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale

**107. Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la Kusimamia na Kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti pamoja na Usimamizi na Uendeshaji mzuri wa Rasilimali Watu katika Wizara. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa Usimamizi Bora wa Mipango na Uendeshaji wa Rasilimali Watu katika Wizara. Programu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi 3,240,624,000/=** na itasimamia programu ndogo tatu ambazo ni: -

i. Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale. (**Shilingi 1,886,738,000/=**)
ii. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara. (**Shilingi 456,249,000/=**)
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba. **(Shilingi 897,637,000/=**)

**108. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ambayo ina jukumu la Kusimamia shughuli zote za Utawala, Utumishi, Maendeleo, Wajibu na Maslahi ya Wafanyakazi wa Wizara.

**109. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Usimamizi na Uendeshaji mzuri wa Rasilimali Watu wa Wizara. Huduma

zinazotarajiwa kutolewa ni Kujenga uwezo na Mazingira Mazuri ya Kazi kwa Wafanyakazi na Usimamizi wa Mpango wa Manunuzi na Fedha.

110. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuweka mazingira mazuri wa kufanya kazi.
ii. Kupima utendaji kazi wa wafanyakazi wa Wizara kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi.
iii. Kusimamia Utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi na kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma na Sheria na Kanuni ya Fedha.
iv. Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA katika utendaji kazi wa Wizara.
v. Kuimarisha mashirikiano baina ya Wadau, Taasisi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa na Wizara kwa ajili ya Maendeleo ya Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

111. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2023/2024, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 833,200,000/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 1,053,538,000/=** kwa ajili ya Mishahara.

112. **Mheshimiwa Spika**, programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la Kupanga, Kutayarisha, Kuratibu, Kufuatilia na Kutathmini Mipango, Sera, Tafiti na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

113. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Kusimamia na Kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti za Wizara. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Uratibu wa Sera na Tafiti, Kuratibu, Kuandaa Bajeti pamoja na Kuratibu na Kusimamia Mipango na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

114. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuratibu Mapitio ya Sera ya Utalii ya mwaka 2017 na kuandaa Mpango wa Utekelezaji
ii. Kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa Idara na Taasisi za Wizara.
iii. Kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Wizara kwa kufuatilia na kutathmini kazi zinazofanyika.
iv. Kuratibu Vikao vya Ushirikiano kwa Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale kati ya SMZ na SMT.
v. Kuandaa maandiko ya miradi yatakayosaidia kupata ufadhili wa miradi inayotekelezwa na Wizara.
vi. Kuratibu Utafiti wa Uwezo wa Zanzibar wa Kuhimili Watalii (Zanzibar Tourism Carrying Capacity).

115. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2023/2024, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla **Shilingi 250,000,000/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 206,249,000/=** kwa ajili ya Mishahara.

116. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba, ina jukumu la Kuhakikisha kuwa Majukumu, Malengo na Shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba.

117. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Kusimamia na Kuratibu shughuli za Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Wizara katika Ofisi Kuu-Pemba. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Uratibu wa Sera, Tafiti na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu-Pemba, Kuratibu Miradi ya Maendeleo na Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi na Mazingira mazuri ya kazi.

118. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuratibu shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba.
ii. Kufuatilia na Kutathmini Utekelezaji wa Malengo na Miradi inayotekelezwa Pemba.
iii. Kuratibu Matamasha ya Utalii yatakayofanyika Pemba.
iv. Kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi vya kutosha ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

119. **Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2023/2024, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 400,000,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 497,637,000/=** kwa ajili ya Mishahara. Aidha, ninaiomba Wajumbe wa Baraza lako iidhinishe makusanyo kwa programu ndogo ya **Shilingi 50,000,000/=.**

## J. SHUKURANI

120. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kutoa shukurani za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kutupa maelekezo na miongozo yenye kuleta matokeo chanya kwa Sekta hizi za Utalii na Mambo ya Kale. Tunaamini kwamba Mheshimiwa

Rais amefanya hivyo kwa lengo la kuhakikisha kwamba Fursa za Utalii na Mambo ya Kale zinawapa faida za moja kwa moja wananchi walio wengi. Tunaahidi kwamba tutaendelea kuthamini na kutekeleza maelekezo yote tutakayopatiwa na Mheshimiwa Rais. Aidha, naomba nitumie fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu Afya, Hekima na Uwezo katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

121. **Mheshimiwa Spika,** shukurani maalumu ziwaendee watendaji Wakuu wa Wizara hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu Bi. Fatma Mabrouk Khamis, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Amina Ameir Issa, Afisa Mdhamini Pemba, Mwenyekiti wa Bodi ya Kamisheni ya Utalii, Ndugu Rahim Bhaloo, Wakurugenzi pamoja na Wakuu wote wa Taasisi za Wizara kwa kuendeleza ushirikiano wa hali ya juu katika kufanikisha malengo na majukumu ya Wizara. Vile vile, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wote wa Wizara hii Unguja na Pemba kwa kuendelea kufanya kazi katika hali ya ubora na umakini wa hali juu, jambo ambalo linapelekea kufanikiwa kwa utekelezaji wa shughuli na malengo ya Wizara kwa ufanisi zaidi.

122. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale wa Unguja na Pemba kwa jinsi tunavyoendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha sekta hizi zinapata maendeleo makubwa na kwa haraka.

123. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Rais Fedha na Mipango pamoja na Tume ya Mipango kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa kuhusu mahitaji na ushauri wa kifedha kwa kipindi chote cha mwaka wa bajeti.

124. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii ya kipekee kukishukuru Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Wananchi wa Jimbo la Tunguu kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono wakati nikitekeleza majukumu yangu.

125. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii ya kipekee kuishukuru familia yangu yote kwa kuanzia na mke wangu kipenzi Bi Kawthar Buwayhid kwa upendo wake, kunisaidia, kunitia moyo na kunivumilia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru wazazi wetu wa pande zote mbili kwa malezi yao yaliyo bora yaliyotuonesha njia sahihi ya maisha na upendo wao ambao umetuwezesha kufika hapa tulipo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awajaalie maisha marefu na yenye afya na kuwaombea kwa Mola aendelee kuzilaza roho za wazazi wetu waliotangulia mbele ya haki malazi mema peponi Amin.

126. **Mheshimiwa Spika,** naomba uniruhusu nizishukuru Nchi, Mashirika na Taasisi ambazo zimeshirikiana kwa karibu na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, katika kufanikisha kutekeleza Malengo na Majukumu ya Wizara kupitia sekta zake mbili. Miongoni mwa nchi hizo ni Oman, Saudi Arabia, India, Urusi, Umoja wa Marekani, Brazil, Ufaransa, Italia, Urusi, China, Uingereza, Ureno, Poland na Qatar pamoja na Mabalozi wote wanaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi.

127. **Mheshimiwa Spika**, Aidha, tunapenda kuyashukuru Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo UNDP, UNESCO, UNICEF, UNECA na UNWTO. Kwa umuhimu wa pekee tunapenda kuzishukuru na kutambua michango ya jumuiya za Kitalii na Mambo ya Urithi na Taasisi za Kifedha, kama vile ZATI, ZATO, ZATOGA, HAZ, TATO, PATI, JUHIMKO, ZAHEFO, PBZ na NMB. Pia, kwa heshima ya kipekee

tunazipongeza timu za Yanga na Simba kwa kuitangaza Tanzania. Vile vile, Tunaipongeza timu ya Yanga kwa kufika fainali ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Kwa kipekee, ninamshukuru Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Utalii na Maliasili wa Tanzania, kwa ushirikiano wake katika kufanikisha majukumu yetu ya pamoja.

128. **Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa Utulivu, Umakini na Usikivu wa hali ya juu.

## K. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

129. **Mheshimiwa Spika,** ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kujadili kwa kina matumizi ya jumla ya Wizara ya **Shilingi 13,984,900,000/=**. Kati ya hizo **Shilingi 2,858,000,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 4,126,900,000/=** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 7,000,000,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo ya mapato ya **Shilingi 1,000,000,000/=** kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.


130. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na Kamisheni ya Utalii katika mwaka wa fedha 2023/2024, imeruhusiwa kutumia fedha zinazotokana na makusanyo. Hivyo, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha makusanyo ya **Shilingi 10,295,888,120/=** ambazo zitakusanywa na Kamisheni ya Utalii, kati ya hizo **Shilingi 4,800,000,000/=** zitaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina, **Shilingi 1,725,888,120/=**

kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 3,770,000,000/=** kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kawaida.

## L. HITIMISHO

**131. Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Waipokee, Waijadili, Watushauri, Watuelekeze na baadae Wapitishe bajeti hii ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

**132. Mheshimiwa Spika**, Naomba Kutoa Hoja.



**Mheshimiwa; Simai Mohammed Said (MBM),**

**Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale.**

**KIAMBATISHO NAMBA 1A**

**FEDHA ZILIZOINGIZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 JULAI 2022-MACHI 2023**

**TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU**

| TAASISI | MAELEZO | BAJETI YA JULAI – JUNI 2022 - 2023 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI – MACHI 2022/2023 |
|---|---|---|---|
| Ofisi kuu Pemba | Mishahara | 366,040,000.00 | 369,050,555.00 |
| | M/Mengineyo | 443,564,000.00 | 94,421,418.00 |
| JUMLA | | 809,604,000.00 | 463,471,973.00 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | 109,741,000.00 | 126,055,130.00 |
| | M/Mengineyo | 300,000,000.00 | 102,251,968.00 |
| JUMLA | | 409,741,000.00 | 228,307,098.00 |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 656,368,000.00 | 746,733,210.00 |
| | M/Mengineyo | 902,727,000.00 | 314,608,628.60 |
| JUMLA | | 1,559,095,000.00 | 1,061,341,838.60 |
| Idara ya Utalii | Mishahara | 244,870,000.00 | 192,383,600.00 |
| | M/Mengineyo | 401,360,000.00 | 82,053,685.11 |
| JUMLA | | 646,230,000.00 | 274,437,285.11 |
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Mishahara | 897,680,000.00 | 959,322,215.00 |
| | M/Mengineyo | 650,450,000.00 | 181,978,600.45 |
| JUMLA | | 1,548,130,000.00 | 1,141,300,815.45 |
| Kamisheni ya Utalii | Mishahara | 848,000,000.00 | 1,112,674,680.00 |
| | M/Mengineyo | 3,025,600,000.00 | 794,595,200.00 |
| JUMLA | | 3,873,600,000.00 | 1,907,269,880.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **JUMLA MISHAHARA** | | **3,122,699,018.00** | **3,506,219,390.00** |
| **JUMLA MATUMIZI MENGINEO** | | **5,723,701,000.00** | **1,569,909,500.16** |
| **JUMLA KU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU** | | **8,846,400,018.00** | **5,076,128,890.16** |

**TAASISI ZA RUZUKU**

| **TAASISI** | **MAELEZO** | **BAJETI YA JULAI – JUNI 2022/2023** | **FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI - MACHI 2022/2023** |
|---|---|---|---|
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | Mishahara | 574,400,000.00 | 607,483,185.00 |
| | M/Mengineyo | 368,300,000.00 | 97,553,667.00 |
| | | 942,700,000.00 | 705,036,852.00 |
| **JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU** | | **574,400,000.00** | **607,483,185.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **368,300,000.00** | **97,553,667.00** |
| **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **942,700,000.00** | **705,036,852.00** |

**TAASISI ZA RUZUKU**

| TAASISI | MAELEZO | BAJETI YA JULAI – JUNI 2022/2023 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI - MACHI 2022/2023 |
|---|---|---|---|
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | Mishahara | 574,400,000.00 | 607,483,185.00 |
| | M/Mengineyo | 368,300,000.00 | 97,553,667.00 |
| | | 942,700,000.00 | 705,036,852.00 |
| **JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU** | | **574,400,000.00** | **607,483,185.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **368,300,000.00** | **97,553,667.00** |
| **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **942,700,000.00** | **705,036,852.00** |
| **JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **3,697,099,018.00** | **4,113,702,575.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO KWA WIZARA** | | **6,092,001,000.00** | **1,667,463,167.16** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA)** | | **9,789,100,018.00** | **5,781,165,742.16** |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | | | |
| Kuimarisha maeneo ya kihistoria | | **7,500,000,000.00** | **492,185,386.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI YA MAENDELEO)** | | **7,500,000,000.00** | **492,185,386.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | **17,289,100,018.00** | **6,273,351,128.16** |

**KIAMBATISHO 1B**

**MAPATO YALIOKUSANYWA JULAI 2022 HADI MACHI 2023**

**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| **TAASISI** | **BAJETI JULAI – JUNI 2022/2023** | **MAPATO YALIOKUSANYWA JULAI 2022 HADI MACHI 2023** | **ASILIMIA** |
|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 700,000,000.00 | 350,103,775.00 | 50.01 |
| Ofisi Kuu Pemba | 50,000,000.00 | 2,536,215.00 | 5.07 |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | 250,000,000.00 | 65,200,000.00 | 26.08 |
| **JUMLA NDOGO** | **1,000,000,000.00** | **417,839,990.00** | **41.78** |
| Kamisheni ya Utalii | 6,200,000,000.00 | 5,124,902,173.00 | 82.66 |
| **JUMLA NDOGO** | **6,200,000,000.00** | **5,124,902,173.00** | **82.66** |
| **JUMLA** | **7,200,000,000.00** | **5,542,742,163.00** | **76.98** |

**KIAMBATISHO 1C**

**FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Programu ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI JULAI – JUNI 2022/2023 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 9,048,130,000.00 | 1,633,486,201.45 | 18.05 |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | 942,700,000.00 | 705,036,852.00 | 74.79 |
| **JUMLA** | **9,990,830,000.00** | **2,338,523,053.45** | **23.41** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kuendeleza Utalii**

| TAASISI | BAJETI JULAI – JUNI 2022/2023 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Utalii | 646,230,000.00 | 274,437,285.11 | 42.47 |
| **JUMLA** | **646,230,000.00** | **274,437,285.11** | **42.47** |

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI JULAI – JUNI 2022/2023 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 1,559,095,000.00 | 1,061,341,838.60 | 68.07 |
| **JUMLA** | **1,559,095,000.00** | **1,061,341,838.60** | **68.07** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamisha Mipango Mikuu ya Wizara**

| TAASISI | BAJETI JULAI – JUNI 2022/2023 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 409,741,000.00 | 228,307,098.00 | 55.72 |
| **JUMLA** | **409,741,000.00** | **228,307,098.00** | **55.72** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI JULAI – JUNI 2022/2023 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 809,604,000.00 | 463,471,973.00 | 57.25 |
| **JUMLA** | **809,604,000.00** | **463,471,973.00** | **57.25** |

**KIAMBATISHO 1D**

## FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 KWA KILA PROGRAMU NDOGO

### Programu ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale

| TAASISI | BAJETI JULAI – JUNI 2022/2023 | FEDHA ILIYOKUSANYWA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 700,000,000.00 | 350,103,775.00 | 50.01 |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | 250,000,000.00 | 65,200,000.00 | 26.08 |
| **JUMLA** | **950,000,000.00** | **415,303,775.00** | **43.72** |

### Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

| TAASISI | BAJETI JULAI – JUNI 2022/2023 | FEDHA ILIYOKUSANYWA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii(Idara ya Mipango) | 6,200,000,000.00 | 5,124,902,173.00 | 82.65 |
| **JUMLA** | **6,200,000,000.00** | **5,124,902,173** | **82.65** |

### Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

| TAASISI | BAJETI JULAI – JUNI 2022/2023 | FEDHA ILIYOKUSANYWA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 50,000,000.00 | 2,536,215.00 | 5.07 |
| **JUMLA** | **50,000,000.00** | **2,536,215.00** | **5.07** |

**KIAMBATISHO 1E**

# BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU

| TAASISI | MAELEZO | BAJETI YA JULAI - JUNI 2023- 2024 |
|---|---|---|
| Ofisi kuu Pemba | Mishahara | 497,637,000.00 |
| | M/Mengineyo | 400,000,000.00 |
| JUMLA | | 897,637,000.00 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | 206,249,000.00 |
| | M/Mengineyo | 250,000,000.00 |
| JUMLA | | 456,249,000.00 |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 1,053,538,000.00 |
| | M/Mengineyo | 833,200,000.00 |
| JUMLA | | 1,886,738,000.00 |
| Idara ya Utalii | Mishahara | 246,877,000.00 |
| | M/Mengineyo | 411,800,000.00 |
| JUMLA | | 658,677,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Mishahara | 1,285,399,000.00 |
| | M/Mengineyo | 650,000,000.00 |
| JUMLA | | **1,935,399,000.00** |
| **JUMLA MISHAHARA** | | **3,289,700,000.00** |
| **JUMLA MATUMIZI MENGINEO** | | **2,545,000,000.00** |
| **JUMLA KU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU** | | **5,834,700,000.00** |

**TAASISI ZA RUZUKU**

| **TAASISI** | **MAELEZO** | **BAJETI YA JULAI - JUNI 2023- 2024** |
|---|---|---|
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | Mishahara | 837,200,000.00 |
| | M/Mengineyo | 313,000,000.00 |
| | | 1,150,200,000.00 |
| **JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU** | | **837,200,000.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **313,000,000.00** |

| | | |
|---|---|---|
| **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **1,150,200,000.00** |
| **JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **4,126,900,000.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO KWA WIZARA** | | **2,858,000,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA)** | | **6,984,900,000.00** |
| Kuimarisha maeneo ya kihistoria | | **7,000,000,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI YA MAENDELEO)** | | **7,000,000,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | **13,984,900,000.00** |

## KAMISHENI YA UTALII

| TAASISI | MAELEZO | BAJETI YA JULAI - JUNI 2023- 2024 |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii | Mishahara | 1,725,888,120.00 |
| | M/Mengineyo | 3,770,000,000.00 |
| | | 5,495,888,120.00 |
| **JUMLA YA MISHAHARA** | | **1,725,888,120.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **3,770,000,000.00** |
| **JUMLA KUU YA KAMISHENI YA UTALII** | | **5,495,888,120.00** |

**KIAMBATISHO 1F**

# BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE
## KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### Programu ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 MATUMIZI | BAJETI 2023/2024 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 8,935,399,000.00 | 700,000,000.00 |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | 1,150,200,000.00 | 250,000,000.00 |
| **JUMLA** | **8,935,399,000.00** | **950,000,000.00** |

### Programu ya Kuratibu na Kuendeleza Utalii

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 MATUMIZI | BAJETI 2023/2024 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Utalii | 658,677,000.00 | - |
| **JUMLA** | **658,677,000.00** | **-** |

## Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 MATUMIZI | BAJETI 2023/2024 MAPATO |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii(Idara ya Masoko) | 890,410,000.00 | - |
| **JUMLA** | **890,410,000.00** | **-** |

## Programu ya Kuratibu na Kusimamia Utalii

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 MATUMIZI | BAJETI 2023/2024 MAPATO |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii(Idara ya Mipango) | 4,605,478,120.00 | 10,295,888,120.00 |
| **JUMLA** | **4,605,478,120.00** | **10,295,888,120.00** |

## Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 MATUMIZI | BAJETI 2023/2024 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 1,886,738,000.00 | |
| **JUMLA** | **1,886,738,000.00** | **-** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamisha Mipango Mikuu ya Wizara**

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 MATUMIZI | BAJETI 2023/2024 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 456,249,000.00 | - |
| **JUMLA** | **456,249,000.00** | **-** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 MATUMIZI | BAJETI 2023/2024 MAPATO |
|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 897,637,000.00 | 50,000,000.00 |
| **JUMLA** | **897,637,000.00** | **50,000,000.00** |

**KIAMBATISHO 1G**

## MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### MAPATO YANAYOINGIA HAZINA

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 |
|---|---|
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | 250,000,000.00 |
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 700,000,000.00 |
| Ofisi Kuu Pemba | 50,000,000.00 |
| **JUMLA NDOGO** | 1,000,000,000.00 |
| Kamisheni ya Utalii | 4,800,000,000.00 |
| **JUMLA NDOGO** | 4,800,000,000.00 |
| **JUMLA** | 5,800,000,000.00 |

**KIAMBATISHO NAMBA 2:**

## WAFANYAKAZI WA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE AMBAO WAMEKWENDA MASOMONI KWA MWAKA 2022/2023

| SHAHA | JINA KAMILI | JINSI | FANI | KIWANGO | MUDA | CHUO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ND. FATMA MALIK ALI | MKE | UTAWALA WA UMMA | SHAHADA YA KWANZA | MIAKA 3 | KAMPALA INTERNATIONAL UNIVERSITY (UGANDA) |
| 2. | ND. TUFAH MUSTAFA ABOUD | MKE | TEHAMA | SHAHADA YA KWANZA | MIAKA 3 | CHUO KIKUU CHA ZANZIBAR (ZU) |
| 3. | ND.ZAINAB KHAMIS KIBWANA | MKE | PANGAJI NA USIMAMIZI WA MIRADI | SHAHADA YA PILI | MIAKA 2 | CHUO CHA UHASIBU ARUSHA |
| 4 | ND. TATU JUMA ALI | MKE | RASILIMALI WATU | SHAHADA YA KWANZA | MIAKA 3 | KAMPALA INTERNATIONAL UNIVERSITY (UGANDA) |
| 5 | ND. ALI JUMA AMEIR | MME | VITU VYA KALE | SHAHADA YA PILI | MIAKA 3 | CHUO KIKUU CHA DAR-ES-SALAAM (UDSM) |
| 6 | ND. TALHIYA SHAMSI AMEIR | MKE | RASILIMALI WATU | SHAHADA YA KWANZA | MIAKA 3 | CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE |
| 7 | ND. ARAFA ISSA AHMADA | MKE | MANUNUZI | STASHAHADA | MWAKA 1 | ICPS |
| 8 | ND. LAILA BAKAR MOH'D | MKE | BUSINESS OPERETION ASISTANCE | CHETI | MWAKA 1 | ICPS |
| 9 | ND. MUZDALIFA MOH'D BAKAR | MKE | UHUSIANO | STASHAHADA | MIAKA 2 | CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA) |
| 10 | ND. KHADIJA SAMI MUSSA | MKE | TEHEMA | ASTASHADA | MWAKA 1 | ICPS |
| 11 | ND. NASSRA HAMAD SALEH | MKE | SANAA NA UTALII | SHAHADA | MWAKA 1 | CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA) |
| **12** | ND. ALI HAMAD ALI | MME | MIPANGO MIJI | SHAHADA YA UZAMIVU | MIAKA 3 | CHUO KIKUU CHA ARDHI DAR-ES-SALAAM |
| 13 | ND. ASHA MMANGA OMAR | MKE | MIPANGO NA UONGOZI | SHAHADA YA UZAMILI | MWAKA 1 | INSTITUTE OF ACCOUNANCY Arusha (IAA) |
| 14 | ND. KHAMIS MZEE ALI | MME | KUMBUKUMBU | STASHAHADA | MIAKA 2 | INSTITUTE OF PROFESSIONAL AND INNOVATIONAL DEVELOPMENT |